

UKENGEUSHI KATIKA UUNDAJI WA ISTILAHU ZA KISWAHILI NA MCHANGO WA KAMUSI

E.K.F. Chiduo

1.0 Utangulizi

Asili ya neno *ukengeushi* ni kitenzi cha Kiswahili *Kengeua*. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981)* inafasiri neno '*kengeua*, kama' "fanya mtu kufuata njia au tabia mbaya; poteza njia, potoa (uk.106)". Hivyo *ukengeushi* ni upotoshaji wa kitu au jambo kwenda au kufanyika bila kufuata kaida zake. Hivyo basi tunaweza kusema kuwa ukengeushi katika uundaji wa istilahi ni uundaji wa istilahi za lugha usiozingatia kaida na ruwaza zilizopo au zilizotangulia kutumika na kuzoeleka.

Uundaji wa istilahi hufanywa kwa lengo la kuziba pengo linalojitokeza la dhana kutoka lugha ya jamiilugha moja na kuingia katika lugha ya jamiilugha nyingine na kukosa istilahi ya kuiwakilisha katika lugha hiyo ya pili.

Lugha nyingi za ulimwengu zina kanuni mahususi za kuunda istilahi za aina mbalimbali ili kukuza msamiati wa lugha hizo kwa lengo la kukidhi mahitaji ya watumiaji wake. Lengo la makala haya ni kuchambua ukengeushi unavyoweza kujitokeza katika uundaji wa baadhi ya istilahi za Kiswahili hususani zinazoundwa kutokana na mnyambuliko wa maneno mengine. Pia, makala yanakusudia kutalii namna kamusi inavyoweza kusaidia kuonyesha mwelekeo wa uundaji wa istilahi za Kiswahili.

1.1 Mbinu za uundaji wa istilahi

Katika ulimwengu, kazi ya kuunda istilahi ilianza karne nyingi ambapo katika Tanzania kazi hiyo ilianza takribani miaka ya 1860 (Massamba, 1996).

Kutokana na kuwa kazi ya kuunda istilahi imefanyika kwa karne kadhaa imekuwa hapana budi kuanzisha vyombo kadhaa vya kushughulikia uundaji wa istilahi. Lakini katika kutekeleza azma hiyo wataalamu wa istilahi wamejaribu kuunda mbinu kadhaa. Mukuthuria (2004) anaeleza kuwa kumekuwapo na mbinu nyingi za kuunda istilahi, lakini anataja mbinu tano tu, ambazo ni: *ukopaji*, *kutafsiri*, *unyambuaji*, *ukatizaji* na *uradidi*.

Mwansoko na Tumbo-Masabo (1992:18) wanafafanua mbinu mbili za kuunda istilahi, ambazo ni *kutafsiri* na *kutumia mifumo ya dhana*. Makala haya yanajikita katika kutumia mbinu hizi mbili katika kuonyesha jinsi unyambulishi wa kitenzi au nomino unaounda istilahi unavyoweza kuunda istilahi ambazo hukengeusha ruwaza za lugha ya Kiswahili.

1.1.1 Kuunda istilahi kwa tafsiri

Mukuthuria (*keshatajwa*) anaelezea namna mbinu hiyo ya kutafsiri, hasa kutoka kwenye lugha ambazo zinajulikana kuwa ni za kimataifa, kama vile Kiingereza, Kifaransa, Kihispania, Kijerumani, Kiarabu na kwenda kwenye lugha lengwa kama vile Kiswahili, inavyofanya kazi. Anasema:

... maneno yanachukuliwa jinsi yalivyo katika lugha chanzi kisha yanawakilishwa na maneno yaliyo na mawazo yanayolingana na yale ya neno la awali kutoka lugha chanz" (uk. 205).

Tafsiri ya baadhi ya maneno yafuatayo ni mifano michache inayodhihirisha mbinu hii:

- | | |
|--------------------------|------------------------------|
| 1. <i>liberalization</i> | - ulegezaji wa masharti |
| <i>industrialization</i> | - ujenzi wa viwanda |
| <i>commercialization</i> | - kufanya kuwa ya kibiashara |

1.1.2 Kuunda istilahi kutokana na mifumo ya dhana

Kwa kulinganisha njia mbili zilizotajwa hapo juu, Mwansoko na Tumbo–Masabo (*weshatajwa*) wamebainisha kuwa njia ya tafsiri ndiyo inayotumiwa sana na vyombo mbalimbali vinavyoshughulika na uundaji wa istilahi.

1.1.3 Unyambulishi wa Kimofolojia

Unyambulishi huunda maneno mapya kwa kuambikwa viambishi kwenye neno, mzizi, au shina la neno. Kwa kufanya hivyo neno, mzizi au shina hubadili umbo lake. Mabadiliko ya namna hii huleta mabadiliko ya *kifahiwa*. Katika Kiswahili, mojawapo ya mbinu ya kupata maneno mapya ni kufanya unyambulishi wa vitenzi na kupata nomino. Tuchunguze mifano ifuatayo:

- | | |
|-------------------|-----------------|
| 2. Kitenzi | Nomino |
| jenga | ujenzi/ujengaji |
| linda | ulinzi/ulindaji |
| sema | usemi/usemaji |

Mnyambuliko ni mchakato ambao hutumika katika lugha nyingi duniani. Katika mifano iliyotolewa hapo juu kiambishi awali u- na kiambishi tamati -i/ji hufanya kitenzi kuwa nomino. Mdee (1990) anasema kuwa vitenzi vya Kiswahili huzalisha sana maneno, kwani mbali na kuzalisha nomino pia huzalisha vitenzi vingine. Angalia mifano ifuatayo:

- | | | | | |
|----------|--------|---------|---------|--------|
| 3. jenga | jengea | jengeka | jengana | jengwa |
| cheza | chezea | chezeka | chezana | chezwa |
| soma | somea | someka | somana | somwa |

Njia nyingine ya kuzalisha nomino ni kutumia kiambishi tamati -o kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

4. penda	pendo
soma	somo
lima	kilimo
kimbia	mbio

1.1.4 Tafsiri kwa mifumo ya Dhana

Katika lugha ya Kiingereza mnyambuliko mmojawapo wa vitenzi unaoweza kubadili kitenzi kuwa nomino ni ule unaotumia viambishi viwili tamati *[-iza.tion/ -ize.ifi]* kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

5. private	-	privatize	-	privat.iza.tion
national	-	nationalize	-	national.iza.tion
standard	-	standardize	-	standard.iza.tion

Kwa kutumia njia ya kwanza hapo juu, yaani kuunda istilahi kwa kutafsiri toka lugha ya Kiingereza, nomino zilizotolewa hapo juu zilipofanyiwa tafsiri katika Kiswahili, tafsiri zake zilikuwa kama ifuatavyo:

6. privat.iza.tion	-	ubinafs.ish.aji
national.iza.tion	-	utaif.ish.aji
standard.iza.tion	-	usanif.ish.aji

Maneno hayo yamefanyiwa tafsiri kwa kufuata mifumo ya dhana kwani ruwaza zake zimefanana. Hii ni mifano michache ya istilahi zilizoundwa kwa tafsiri. Hapa kuna dalili kuwa vyombo vinavyohusika katika uundaji wa istilahi vilitumika kufikia maamuzi hayo na hivyo kuweka msingi wa tafsiri za maneno yenye ruwaza ya aina moja kutoka lugha chanzi na pia kuendelea kuwa na ruwaza ya aina hiyo kwenye lugha lengwa.

1.1.5 Tafsiri Iliyokengeushwa

Baadhi ya maneno katika lugha ya Kiswahili yaliyofanyiwa tafsiri toka Kiingereza yamekengeuka kutokana na kutofanyiwa tafsiri ipasavyo au kwa kutozingatia misingi na mbinu za uundaji wa istilahi kulingana na dhana zilizomo katika maneno hayo. Baadhi ya mifano ni kama ifuatayo:

7. global.iza.tion	-	utandawazi
liberal.iza.tion	-	ulegezaji wa masharti
industrial.iza.tion	-	ujenzi wa viwanda

Tafsiri ya Kiswahili kwa maneno haya imekengeuka kwani haikufuata ruwaza ya tafsiri za maneno kama yaliyoonyeshwa hapo juu (taz. 2.1) kwani matarajio ni kuwa maneno hayo yangukuwa na tafsiri zenye misingi ya dhana na ruwaza lakini sivyo ilivyojitokeza. Mifano ifuatayo ni mapendekezo ambayo kama maneno haya yangeshughulikiwa kwa kufuata msingi wa dhana na ruwaza basi zingeweza kupatikana istilahi kama hizi:

- | | | |
|---------------------|---|------------------|
| 8. global.iza.tion | - | utandawa.ish.aji |
| liberal.iza.tion | - | uhuri.ish.aji |
| industrial.iza.tion | - | utasni.ish.aji |
| commercial.iza.tion | - | ubiashar.ish.aji |

Matarajio hayo yalikuwa hivyo kutokana na msingi kuwa ruwaza ya [-ization] katika Kiingereza imepata mashiko ya [-ishaji] katika Kiswahili na hivyo ni matarajio kuwa wakuza istilahi wangepaswa kutumia mbinu ya kuambatisha viambishi tamati vya [-ish.aji] katika maneno yote ya Kiingereza yanayoibuka na yenye ruwaza kama iliyotajwa hapo juu na ambayo hayana visawe vyake katika Kiswahili. Tumbo (1982) anabaini kuwa kuna mapendekezo kuwa uundaji wa istilahi unaweza kuanza na tafsiri lakini tafsiri isiwe ndiyo mwisho bali wataalamu wa uundaji wa istilahi waitumie kama nyenzo ya kuelekea kutumia mifumo ya dhana. Tukitumia mfano wa neno *utandawazi* kwa tafsiri ya neno *globalization*, hiyo inaonyesha hatua ya awali ya kutumia tafsiri tu katika kuiunda istilahi hiyo. Endapo mbinu ya kutumia mifumo ya dhana ingelitumika wataalamu wa uundaji istilahi wangepikiria pia mambo mengi zaidi, kwa mfano, wangeligawa neno *globalization* katika mofimu mbili ambazo zinawakilisha dhana mbili. Hii inakubaliana na msingi mmoja muhimu kama ulivyofafanuliwa na Felber (1980), Sager na Johnson (1978) unaosema kuwa uhusiano baina ya dhana ndiyo uwe msingi wa uundaji wa istilahi. Dhana mbili zilizomo katika neno *globalization* zinawakilishwa na mofimu mbili kama zifuatazo:

Dhana ya *global* yaani *-a ulimwengu*: Jambo linalohusu ulimwengu wote. Hapo ile fahiwa ya kutanda au utandawaa, yaani kuenea sehemu zote, ingekuwa imewakilishwa vizuri.

Dhana [-ization] kutoka katika lugha ya Kiingereza: Dhana hii inawakilishwa katika lugha ya Kiswahili na umbo la [-ishaji] kwa maana ya kuonyesha kuwa mchakato wa kufanya ueneaji au utandawaji huo kuwa unaendelea na haujafikia mwisho. Neno *Utandawazi* linatoa dhana kuwa hakuna mchakato unaoendelea bali huonyesha kuwa kuna *uwazi umetanda* au *upo kila mahali katika eneo linalohusika ambalo ni ulimwengu mzima*. Neno hili halileti mantiki kwa kuwa *utandawazi* si jambo linalomfikia kila mtu kwa wakati mmoja bali kila mtu au kundi la watu hufikiwa kwa wakati maalumu baada ya mazingira sahihi kuwepo mahali hapo. Kwa mfano, leo katika Tanzania hatuwezi kusema

nchi imefikia utandawazi wakati ambapo mazingira yanayoweza utandawazi kuwapo hayajakamilika. Hivyo dunia haiko kwenye utandawazi bali iko kwenye utandawashaji kama mchakato wa kufikia malengo. Mwansoko na Tumbo-Masabo (*weshatajwa*) wanaita uundaji wa istilahi wa namna hii, “mparaganyiko unaosababishwa na misingi mibovu na/au isiyotimilika ya uundaji na usanifishaji wa istilahi”.

Akiunga mkono umuhimu wa kufuata ruwaza zenye mashiko katika kuunda istilahi au kunyambua maneno, Atchison (1996) anaufananisha utaratibu huo na mito ambayo haiwezi kutiririka kwa kurudi nyuma ilikotokea, yaani kinyumenyume. Anasema lugha pia hutiririka kufuata mwelekeo unaotabirika.

2.0 Mchango wa Kamusi katika Kutunga Istilahi

Kwa kawaida watunga istilahi wanapaswa kuwa watalaamu wa lugha. Hivyo kabla ya kutunga na kuitumia istilahi wanapaswa kutumia marejeo mbalimbali. Mojawapo ya marejeo muhimu ni kamusi zilizopo. Zgusta (1971) amefasili kamusi kuwa ni kitabu cha marejeo chenye msamiati uliokusanywa kutoka kwa wazungumzaji wa jamii fulani na kupangwa katika utaratibu maalumu na kufafanuliwa kwa namna ambayo msomaji anaweza kuelewa maana iliyokusudiwa.

2.1 Kamusi Sanifu ya Kiingereza-Kiswahili (Johnson, 1939)

Katika kuunda istilahi ya Kiswahili kutokana na istilahi za kutoka lugha nyingine, hususani Kiingereza, mtunga istilahi anapaswa kutunga istilahi inayochukua ruwaza ambazo tayari zina mashiko ndani ya lugha. Mwongozo huo anaweza kuupata ndani ya kamusi kama kamusi inayohusika imeingiza maneno na istilahi kwa kuzingatia ruwaza inayofaa. Ifuatayo ni mifano michache inayoonyesha jinsi kamusi zinavyoweza kuchangia katika uundaji wa istilahi bora au istilahi zilizokiuka taratibu na ruwaza za lugha ya Kiswahili. Tuanze na mifano ya ukiukaji taratibu na ruwaza. Tuangalie maneno yafuatayo yalivyoingizwa na kutolewa taarifa zake katika kamusi ya *Kingereza-Kiswahili* ya Johnson ya mwaka 1939.

commercial, - a kuhusu biashara na wafanyibiashara. *The Commercial world* watu wa biashara. *Commercial matters, dealings* mambo ya biashara. *Commercial traveller* mtu asafiriye kuonyesha vitu vya biashara na kupokea maagizo juu yake (uk. 100).

devitalize, *v.t.* ondoa uzuri (uhai, nguvu), dhoofisha (uk. 147).

harmony, *n.* amani, mapatano, upatano, umoja, moyo
mmoja **harmonize**, *v.t.* patanisha, linganisha;
_____ *v.i* lingana, patana, chukuana. (uk. 257).

- mobility, n.** wepesi wa kugeuka, mwendo. **mobilize, vt** kusanya (askari, baharia, zana za vita) tayari kwenda vitani (uk. 351).
- stable,** a. *thabiti, imara, hodari,...* **stabilize, v.t.** imarisha thibitisha, kaza (uk. 529).
- standard, n.** (*flag*) bendera **standardization, n...** (uk. 531).

Tukichunguza vidahizo hivi tunaona kuwa vyote havikuweza kufikisha ufafanuzi wake mahali panapostahili, yaani baadhi ya vinyambuo havikutolewa maana. Kidahizo **devitalize** hakikamilishi unyambulishi wake hadi kufikia nomino **devitalization** ambayo kisawe chake cha Kiswahili kingekuwa kimetolewa yaani *udhoofishaji*. Pia kidahizo **harmony** hakikumaliza unyambulishi na kufika kwenye nomino **harmonization** ambayo kisawe cha Kiswahili kingeonyeshwa kuwa ni *upatanishaji*. Vivyo hivyo kinyambuo cha nomino cha neno **commercial** ambacho ni **commercialization** hakikuonyeshwa na hivyo kutotoa nafasi kwa mtumiaji wa Kiswahili kupata kisawe cha neno hili kwa Kiswahili. Neno **mobilize** limeingizwa ndani ya kidahizo **mobility**, hata hivyo mwendelezo huo haukukamilika kwa kuwa neno **mobilization** ambalo ni mnyambuliko wake halikuingizwa.

Katika mifano iliyotolewa hapo juu ni kidahizo **standard** ambacho kimepiga hatua moja mbele ya unyambulishi kwa kuingiza nomino **standardization**. Hata hivyo kinyambuo hicho hakikupewa maana katika Kiswahili. Itamlazimu mtumiaji wa kamusi, hususani mfasiri, aunde istilahi ya Kiswahili kwa kuangalia maana kama ilivyotolewa katika neno la msingi. Hii inahitaji utalaamu, zaidi ya kuwa mfasiri. Matokeo yake dhana moja inakuwa na fasiri nyingi kutokana na wafasiri wengi kuipatia visawe tofauti.

2.2 Kamusi ya Kiingereza - Kiswahili (TUKI, 1996)

Maneno hayo tuyaangalie yalivyofafanuliwa maana zake katika kamusi ya Kiingereza – Kiswahili (TUKI, 1996).

- devitalize vt** *ondoa nguvu, dhoofisha, fifisha, fifiliza, devitalization* n.(uk. 201).
- harmony n. 1.** *upatanifu (katika maono mtazamo n.k.), amani. 2. (music) mwafaka, ulinganifu wa sauti harmonization n* (uk. 355).
- mobilize vt, vi** andaa watu kufanya jambo, hamasisha. **mobilization n** (uk. 498).
- stable adj** *thabiti, imara, tulivu,...* **stabilization n. Stabilize vt.** dhibiti, tengemeza, tuliza, imarisha.... (uk. 740).

thought and action utulivu wa mawazo na vitendo (uk. 440).

mobilize, mobilise [] *vb*: - hamasisha watu (uk. 623).

mobilization, mobilisation [] *n*: uhamasishaji wa watu

stable *adj* 1. (= *steady*) imara; **this chair isn't very ~** kiti hiki si imara ana; 2. *fig*: imara 4. *econ*: imara; ~ **currency** sarafu imara (uk. 890).

standard [] *n* 1. bendera (-); bango (*ma-*) lenye maandishi; 2. kiwango (*vi-*) (*ex maintain a high standard*); ...

Katika vidahizo vya hapo juu hakuna kidahizo ambacho kilifanyiwa unyambulishi na kufikia hatua ya [-ization] katika Kiingereza. Kamusi hii haikusaidia kuziba pengo la kisemantiki lililokuwapo katika kamusi zilizotangulia. Leksimu **mobilization** imeingizwa kama kidahizo cha pekee bila kuwa chini ya **mobilize**. Hii inaonyesha udhaifu wa kutokuwa na ruwaza moja katika uingizaji wa leksimu. Kama uingizaji wa taarifa ungefanywa kwa umakini leksimu kama *harmonization, stabilization* na *standardization* zingeingizwa chini ya vidahizo vinavyohusika kwani visawe vyake ambavyo ni *upatanishaji, uimarishaji, na usanifishaji* kwa mfuatano huo, vilikuwa tayari vinatumiwa na wazungumzaji na waandishi wa Kiswahili wakati kamusi hii ilipokuwa inachapishwa, lakini haikufanyika hivyo.

3.0 Hitimisho

Makala haya yamejadili ukengeushi katika utungaji wa istilahi. Makala yamesisitiza kuwa ukengeushi unatokana na kutozingatia ruwaza za maneno yaliyozoeleka na yenye mashiko katika lugha. Ruwaza iliyochambuliwa ni ya [-ishaji]. Pia ukengeushi unatokana na kufanya tafsiri za maneno ya kigeni bila kuzingatia dhana zinazoashiriwa na maneno hayo. Uzingatiaji wa dhana kuu ndio unapaswa kuwa msingi wa kutunga istilahi mpya.

Kamusi tatu zimechunguzwa na kudhihirika kuwa, nazo kwa namna fulani haziwezi kusaidia sana katika kuingiza kwa uwazi zaidi istilahi zinazotokana na minyambuo kwa kuzingatia ruwaza maalumu. Kamusi ya *Kiingereza – Kiswahili* ndiyo imeweza kuingiza minyambuo ya nomino ya Kiingereza lakini haikuingiza visawe vya Kiswahili. Kamusi ya Johnson (1939) na Kirkeby (2000) hazikushughulikia vinyambuo vya nomino kwa kiwango kilichofikiwa na Kamusi ya *Kiingereza – Kiswahili* ya TUKI (1996).

MAREJEO

- Aitchison, Jean (1996). *Words in the Mind* Oxford: Blackwell.
- Chiduo, E.K.F. (1997). "Synonymy in the Standard Swahili Dictionary", unpublished Doctoral Dissertation, Columbia University, New York.
- Kirkeby, Willy A. (Ed.) (2000), *English – Swahili Dictionary*. Dar es Salaam, Kakepela Publishing,
- Masabo, Tumbo Z.N.Z. na Mwansoko H.J.M. (1992). *Kiongozi cha Uundaji wa Istilahi za Kiswahili, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Massamba, D.P.B. (1996). "Problems in Terminology Development: The case of Tanzania" katika *Kiswahili Vol. 59*, Institute of Kiswahili Research, University of Dar es salaam.
- Massamba, D.P.B. (1995). "Lahaja na Mitindo katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu", katika Kiango, J.G. (mh.) 1995, *Dhima ya Kamusi katika Kusanifisha lugha*, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es salaam.
- Mukuthuria, M. (2004). "Kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru: Mfano kutokana na wanafunzi wa Tigania, Kenya", Chuo Kikuu cha Egerton- Kenya
- TUKI (1996). *English – Swahili Dictionary*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research University of Dar es Salaam.
- TUKI (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam na Nairobi: Oxford University Press.
- Tumbo, Z. (1982). "Towards a Systematic Terminology Development in Kiswahili", *Kiswahili, Juz. 49/1*, Institute of Kiswahili Research, University of Dar es Salaam.
- Zgusta, L. (1971). *Manual of Lexicography*, Mouton, The Hague.